WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA

UJENZI WA CHUO CHA VETA MKOA (RVTSC)

MKOA WA SIMIYU

# MKATABA WA MUDA MFUPI WA KAZI YA UFUNDI

**MKATABA HUU NI KATI YA**

**CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI BARIADI**

**BARIADI FDC**

**NA**
**ELIUDI JOHN MLENZA**
**(FUNDI)**

**JINA LA MRADI**
**UJENZI WA CHUO CHA VETA MKOA**
**SIMIYU RVTSC – SIMIYU**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI
BARIADI

# MKATABA WA UJENZI WA KAZI YA UASHI

1. MWAJIRI: CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI BARIADI
   S.L.P. 16 BARIADI
2. JINA LA MWAJIRIWA (FUNDI UASHI): ELIUDI JOHN MLENZA
3. MAHALI KAZI ITAKAPOFANYIKA: MKOANI SIMIYU
4. KAZI: UJENZI WA MABWENI MANNE (04) NA JENGO LA UTAWALA (LOT 1)
5. **GHARAMA YA UFUNDI: SHILINGI MILIONI MIA MOJA SABINI NA TANO LAKI TATU TU. ( TZS: 175,300,000/=)**
6. **AINA YA MKATABA: MKATABA WA KUFANYA KAZI YA UFUNDI**
7. **MUDA WA MKATABA: MIEZI SITA (06)**
8. **MASHARTI YA MALIPO:**
   **a) Hakuna malipo ya awali**
   **b) Fundi atalipwa mara baada ya kazi kukaguliwa na hati ya malipo (*payment certificate*) kuandaliwa.**
9. **MASHARTI YA MKATABA:**

a) Mwajiri atatoa vifaa vya ujenzi kwa namna na jinsi atakavyoelekezwa na Mtaalam Mshauri wa Mradi.

b) Maelekezo ya kazi yatatolewa na msimamizi mkuu wa kazi *(Clerk of works)* na mwajiriwa (Fundi) ataomba malipo fedha kwa kazi aliyoifanya kwa mkuu wa Chuo kupitia msimamizi wa kazi na atalipwa endapo ukubwa wa kazi aliyofanya itakaguliwa na kufika angalau 40%.

c) Mwajiriwa, ambaye ambaye kwenye Mkataa huu atajulikana kama Fundi Mkuu katika utendaji wa kazi, atafanya kazi kwa mujibu wa Mchanganuo wa Kazi kwa kuzingatia taaluma ya ufundi, umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.

d) Mwajiriwa asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumwondoa kwenye kazi na papo hapo na kumdai kulipa hasara zote zilizotokana na uzembe au makusudi.

e) Mwajiriwa atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanya kulingan na taratibu za kiujenzi.

f) Mwajiriwa, wakati wote, atahakikisha kuwa yeye pamoja na mafundi wenzake atazingatia nidhamu na tabia njema awapo eneo la kazi na haruhusiwi kabisa kuajiri fundi au kibarua asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.

g) Mwajiriwa atawajibika na vitendo vyote vinavyofanywa au kutokufanywa na mafundi au vibarua waliopo chini yake.

h) Mwajiriwa atahakikisha kuwa wakati wote eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki ataviweka sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.

i) Kiasi cha asilimia tano (5%) ya malipo kitashikiliwa na Mwajiri *(Retention Money)* kwa muda wa miezi mitatu (03) baada ya kazi kukamilika na nakulipwa iwapo ukaguzi wa mwisho utathibitisha kutokuwepo mapungufu ya kurekebisha.

j) Iwapo mapungufu yatabainika wakati wa ukaguzi, Mwajiriwa atahitajika kurekebisha mapungufu hayo na baada ya hapo atamaliziwa kiasi kilichosalia ikiwa mapungufu yaliyorekebishwa hayakuleta hasara kwa Mwajiri.

k) Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na Mwajiriwa ni ukiukwaji wa Mkataba huu hivyo Mwajiriwa atakatwa asilimia moja (1%) ya fedha iliyo katika mkataba kwa kila siku inayoongezeka au kulipa kiasi cha fedha sawa na hasara iliyosababishwa kutokana na ucheleweshwaji huo.

l) Ucheleweshwaji utakaosababishwa na Mwajiri au sababu zilizo nje ya uwezo wa mwanadamu *(act of God/force majeure)*, Mwajiriwa ataongezewa muda ili akamilishe kazi pasipo kudai fidia yoyote.

m) Mkataba huu unaweza kuvunjwa mara moja kwa mambo yafuatayo:

a) Iwapo fundi Mkuu au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Mwajiri na Mwajiriwa akashindwa kutoa ushirikiano wakati wa uchunguzi wa tukio la wizi;

b) Iwapo Fundi Mkuu au Mafundi walioko chini yake watafanya kazi bila kufuata mchoro au maelekezo ya Mshauri na Msimamizi wa Mradi na Mwajiriwa akawa ni miongoni mwa waliohusika au kushindwa kumtaarifu Mwajiri juu ya suala hilo;

c) Iwapo Fundi Mkuu au Mafundi walioko chini yake hawatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi na ikabainika kuwa Mwajiriwa hakujishughulisha na kuhakikisha kuwa taratibu zinafatwa;

d) Iwapo Fundi Mkuu au Mafundi au Vibarua watahatarisha uvunjifu wa amani eneo la kazi.

10.1: MABWENI MANNE

| Na. | AINA YA KAZI | BEI YA UFUNDI - TZS |
|---|---|---|
| A | Msingi wa Jengo (Sub-structure) | |
| | Kuseti jengo. | 500,000.00 |
| | Uchimbaji wa msingi pamoja na shimo la nguzo. | 1,000,000.00 |
| | Kufukia na kushindilia Msingi. | 800,000.00 |
| | **Usukaji wa Nondo katika;** | |
| | Nguzo Mlalo za kwenye msingi (Ground beams) | 300,000.00 |
| | Uwekaji wa BRC Mesh eneo la Jamvi | 500,000.00 |
| | **Kufunga na kuondoa mbao:** | |
| | Pembezoni mwa jamvi | 600,000.00 |
| | **Kumwaga zege:** | |
| | Chini kwenye kitako cha msingi (Strip foundation footing) | 600,000.00 |
| | Katika nguzo Mlalo za kwenye Msingi (ground beams) | 600,000.00 |
| | Kwenye jamvi (oversite concrete) | 1,200,000.00 |
| | Umwagiliaji wa maji (Curing) | 250,000.00 |
| | **Kuta za Msingi:** | |
| | Ujenzi wa kuta za msingi | 2,000,000.00 |
| | **Upangaji na ushindiliaji;** | |
| | Upangaji wa mawe na utandazaji wa DPM | 1,500,000.00 |
| | Uwekaji wa kifusi | 800,000.00 |
| | Uwekaji wa sumu ya mchwa | 300,000.00 |
| | **Jumla ndogo msingi wa jengo-A** | **10,950,000.00** |
| **B.** | **Kunyanyua jengo (Super-structure):** | |
| | Ujenzi wa kuta,gebo na matundulizi na uwekaji DPC | 2,500,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| | Kusuka nondo katika: | |
| | Nguzo mlalo ya kwanza (Beam) | 300,000.00 |
| | Nguzo mlalo ya Pili (Beam) | 300,000.00 |
| | Ngazi na Ramp | 300,000.00 |
| | | |
| | **Kufunga mbao katika:** | |
| | Nguzo mlalo ya Kwanza (Beam) | 300,000.00 |
| | Nguzo mlalo ya Pili (Beam) | 300,000.00 |
| | Ngazi na Ramp | 200,000.00 |
| | | |
| | **Kumwaga zege katika:** | |
| | Nguzo mlalo ya Kwanza (Beam) | 500,000.00 |
| | Nguzo mlalo ya Pili (Beam) | 500,000.00 |
| | Ngazi na Ramp | 450,000.00 |
| | | |
| | **Jumla ndogo Kunyanyua jengo (Super-structure)-B** | **5,650,000.00** |
| | | |
| **C.** | **Kuezeka (Roof structure and covering)** | |
| | Kutengeneza kenchi za mbao kwa kufuata mchoro | 750,000.00 |
| | Kupandisha kenchi za mbao kwenye jengo | 500,000.00 |
| | Kuezeka | 250,000.00 |
| | **Jumla ndogo Kuezeka-C** | **1,500,000.00** |
| | | |
| **D.** | **Milango:** | |
| | Kufitisha fremu za milango | 800,000.00 |
| | **Jumla ndogo Milango - D** | **800,000.00** |
| | | |
| **E.** | **Madirisha:** | |
| | Kufitisha grill za madirisha | 800,000.00 |
| | **Jumla ndogo Madirisha-E** | **800,000.00** |
| | | |

| | | |
|---|---|---|
| F. | Umaliziaji (Finishing) | |
| | Upigaji wa lipu pamoja na kutengeneza koplo | |
| | Nje ya jengo | 800,000.00 |
| | Ndani ya jengo | 600,000.00 |
| | | |
| | **Sakafu:** | |
| | Uwekaji wa sakafu ya kupokea vigae (beds) | 700,000.00 |
| | Uwekaji wa vigae pamoja na grauti katika sakafu (floor tiles) | 500,000.00 |
| | Uwekaji wa vigae pamoja na grauti katika Kuta maeneo ya Jikoni na Vyooni (Wall tiles) | 500,000.00 |
| | | |
| | **Dari:** | |
| | Ufungaji wa mbao za dari (Brandering) | 800,000.00 |
| | Uwekaji gypsum ceiling pamoja na mikanda yeke | 600,000.00 |
| | | |
| | **Jumla ndogo umaliziaji(finishing)-F** | **4,500,000.00** |
| | | |
| **G.** | **Rangi na Mapambo (Painting & Decoration)** | |
| | **Kupaka rangi mikono mitatu pamoja na skimming katika:** | |
| | Nje ya jengo | 600,000.00 |
| | Ndani ya jengo | 600,000.00 |
| | Juu ya dari | 300,000.00 |
| | | |
| | **Kupaka rangi mikono mitatu katika:** | |
| | Msingi wa nyumba | 300,000.00 |
| | Fisherboard na Roof Vents | 300,000.00 |
| | **Jumla ndogo Rangi na mapambo-G** | **2,100,000.00** |
| | | |
| **H.** | **Umeme (Electrical installation)** | |
| | Usukaji wa umeme awamu ya kwanza - Conduit na Box | 600,000.00 |
| | Usukaji wa umeme awamu ya pili (2nd fix)-fittings | 600,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| | Jumla ndogo Umeme-H | 1,200,000.00 |
| | | |
| I | Mifumo ya maji safi na taka (Water Supply and Sewage system) | |
| | Ufungaji bomba awamu ya kwanza (Kuchimbia bomba) | 600,000.00 |
| | Ufungaji bomba awamu ya pili (2nd fix) -fittings | 600,000.00 |
| | Uchimbaji wa mashimo ya maji taka (Septic na Soak pit) | 600,000.00 |
| | Ujenzi wa mashimo ya maji taka na chemba zake ikiwa ni pamoja nakufanyia finishings | 750,000.00 |
| | **Jumla ndogo Mifumo ya maji safi na maji Taka-I** | **2,550,000.00** |
| **SUMMARY** | | |
| A | Gharama za Msingi (Substructure) | 10,950,000.00 |
| B | Gharama za Kunyanyua Jengo(Superstructure) | 5,650,000.00 |
| C | Gharama za Kuezeka | 1,500,000.00 |
| D | Gharama za Kufutisha Milango | 800,000.00 |
| E | Gharama za Kufutisha Madirisha | 800,000.00 |
| F | Gharama za Umaliziaji (Finishing) | 4,500,000.00 |
| G | Gharama za Rangi na Mapambo | 2,100,000.00 |
| H | Gharama za Umeme | 1,200,000.00 |
| I | Gharama za Mifumo ya Maji Safi na Maji Taka | 2,550,000.00 |
| **JUMLA KUU YA GHARAMA ZA KAZI ZA UJENZI KWA BWENI MOJA** | | **30,050,000.00** |
| **IDADI YA MAJENGO (DORMITORY)** | | **4** |
| **JUMLA KUU MABWENI MANNE (04)** | | **120,200,000.00** |

10.2: JENGO LA UTAWALA

| Na. | AINA YA KAZI | BEI YA UFUNDI - TZS |
|---|---|---|
| A | Msingi wa Jengo (Sub-structure) | |
| | Kuseti jengo. | 500,000.00 |
| | Uchimbaji wa msingi pamoja na shimo la nguzo. | 1,000,000.00 |
| | Kufukia na kushindilia Msingi. | 300,000.00 |
| | | |
| | **Usukaji wa Nondo katika;** | |
| | Kitako cha nguzo (Column base) | 800,000.00 |
| | Nguzo wima za Msingi (Column starter) | 800,000.00 |
| | Nguzo Mlalo za kwenye msingi (Ground beams) | 600,000.00 |
| | Uwekaji wa BRC Mesh eneo la Jamvi | 800,000.00 |
| | | |
| | **Kufunga na kuondoa mbao:** | |
| | Pembezoni mwa jamvi | 300,000.00 |
| | Pembezoni mwa nguzo wima za Msingi, Pembezoni mwa nguzo Mlalo za Msingi pamoja na pembeni mwa Kitako cha nguzo (Column base) | 500,000.00 |
| | | |
| | **Kumwaga zege:** | |
| | Chini kwenye kitako cha msingi (Strip foundation footing) | 800,000.00 |
| | Chini kwenye kitako cha nguzo (Blinding) na kwenye kitako cha nguzo (Column base) | 600,000.00 |
| | Katika nguzo wima za awali (Column starter) | 600,000.00 |
| | Katika nguzo Mlalo za kwenye Msingi (ground beams) | 600,000.00 |
| | Kwenye jamvi (oversite concrete) | 1,500,000.00 |
| | Umwagiliaji wa maji (Curing) | 300,000.00 |
| | | |
| | **Kuta za Msingi:** | |
| | Ujenzi wa kuta za msingi | 1,200,000.00 |
| | | |
| | **Upangaji na ushindiliaji;** | |
| | Upangaji wa mawe na utandazaji wa DPM | 800,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| | Uwekaji wa kifusi | 500,000.00 |
| | Uwekaji wa sumu ya mchwa | 300,000.00 |
| | **Jumla ndogo msingi wa jengo** | 12,800,000.00 |
| **B.** | **Kunyanyua jengo (Super-structure):** | |
| | Ujenzi wa kuta na uwekaji DPC sakafu ya chini (ground floor) | 1,400,000.00 |
| | Ujenzi wa kuta za urembo (Fin wall) sakafu ya chini ya kwanza (ground floor & First Floor) | 800,000.00 |
| | **Kusuka nondo katika:** | |
| | Nguzo mlalo sakafu ya chini (Ground floor) | 400,000.00 |
| | Nguzo wima sakafu ya chini (Ground floor) | 400,000.00 |
| | Sakafu ya kwanza (First floor slab) | 600,000.00 |
| | Ngazi, Ramp pamoja na Matega maji ya mvua (Gutter) | 300,000.00 |
| | **Kufunga mbao katika:** | |
| | Nguzo mlalo sakafu ya chini (Ground floor) | 300,000.00 |
| | Nguzo wima sakafu ya chini (Ground floor) | 300,000.00 |
| | Sakafu ya kwanza (First floor slab) | 800,000.00 |
| | Ngazi, Ramp pamoja na Matega maji ya mvua (Gutter) | 150,000.00 |
| | **Kumwaga zege katika:** | |
| | Nguzo mlalo sakafu ya chini (Ground floor) | 800,000.00 |
| | Nguzo wima sakafu ya chini (Ground floor) | 800,000.00 |
| | Sakafu ya kwanza (First floor slab) | 1,200,000.00 |
| | Ngazi, Ramp za chini pamoja na Matega maji ya mvua (Gutter) | 500,000.00 |
| | **Sakafu ya kwanza (First floor):** | |
| | Ujenzi wa kuta sakafu ya kwanza (First floor) | 1,200,000.00 |
| | Ujenzi wa kuta za juu ya paa (Parapet wall) | 600,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| | Jumla ndogo Kuezeka | |
| | | 2,100,000.00 |
| D. | Milango: | |
| | Kufitisha fremu za milango | 800,000.00 |
| | **Jumla ndogo Milango** | |
| | | **800,000.00** |
| **E.** | **Madirisha:** | |
| | Kufitisha grill za madirisha | 1,000,000.00 |
| | **Jumla ndogo Madirisha** | |
| | | **1,000,000.00** |
| **F.** | **Umaliziaji (Finishing)** | |
| | **Upigaji wa lipu pamoja na kutengeneza koplo** | |
| | Nje ya jengo sakafu ya chini (Ground floor) | 1,000,000.00 |
| | Ndani ya jengo sakafu ya chini (Ground floor) | 1,300,000.00 |
| | Juu ya dari ya zege (concrete ceiling) sakafu ya chini (Ground floor) | 500,000.00 |
| | | |
| | **Sakafu ya kwanza (First floor):** | |
| | Nje ya jengo sakafu ya kwanza (First floor) | 800,000.00 |
| | Ndani ya jengo sakafu ya kwanza (First floor) | 800,000.00 |
| | | |
| | **Sakafu:** | |
| | Uwekaji wa sakafu ya kupokea vigae (beds) sakafu ya chini (Ground floor) | 800,000.00 |
| | Uwekaji wa vigae pamoja na grauti katika sakafu (floor tiles) - sakafu ya chini (Ground floor) | 1,000,000.00 |
| | Uwekaji wa vigae pamoja na grauti katikaKuta maeneo ya Vyooni (Wall tiles) - sakafu ya chini (Ground floor) | 500,000.00 |
| | | |
| | **Sakafu ya kwanza (First floor):** | |
| | Uwekaji wa sakafu ya kupokea vigae (beds) sakafu ya kwanza (First floor) | 500,000.00 |
| | Uwekaji wa vigae pamoja na grauti katika sakafu (floor tiles) - sakafu ya kwanza (First floor) | 800,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| | Uwekaji wa vigae pamoja na grauti katikaKuta maeneo ya Vyooni (Wall tiles) - sakafu ya kwanza (First floor) | 350,000.00 |
| | | |
| | **Dari:** | |
| | Ufungaji wa mbao za dali (Brandering) | 800,000.00 |
| | Uwekaji strips (Main T, wall angle na cross member) pamoja na dali (False ceilingi) | 800,000.00 |
| | | |
| | **Jumla ndogo umaliziaji(finishing)** | **9,950,000.00** |
| | | |
| G. | **Rangi na Mapambo (Painting & Decoration)** | |
| | **Kupaka rangi mikono mitatu pamoja na skimming katika:** | |
| | Nje ya jengo sakafu ya chini (Ground floor) | 1,000,000.00 |
| | Ndani ya jengo sakafu ya chini (Ground floor) | 1,200,000.00 |
| | Juu ya dari ya zege (concrete ceiling) sakafu ya chini (Ground floor) | 350,000.00 |
| | | |
| | **Sakafu ya kwanza (First floor):** | |
| | Nje ya jengo sakafu ya kwanza (First floor) | 600,000.00 |
| | Ndani ya jengo sakafu ya kwanza (First floor) | 400,000.00 |
| | | |
| | **Kupaka rangi mikono mitatu katika:** | |
| | Msingi wa nyumba | 300,000.00 |
| | Fisherboard na Roof Vents | 300,000.00 |
| | **Jumla ndogo Rangi na mapambo** | **4,150,000.00** |
| | | |
| H. | **Umeme (Electrical installatión)** | |
| | Usukaji wa umeme awamu ya kwanza - Conduit na Box | 500,000.00 |
| | Usukaji wa umeme awamu ya pili (2nd fix)-fittings | 1,000,000.00 |
| | **Jumla ndogo Umeme** | **1,500,000.00** |
| | | |
| I | **Tehama** | |

MWAJIRI

Saini ..........................................

Jina BEATHA RUTELANO

Cheo KN MKUU WA CHUO

Tarehe 23/11/2021

MKUU WA CHUO
CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI
BARIADI

SHAHIDI WA MWAJIRI

Saini ...Bhaula.

Jina BEATRICE F. CHAULA

Cheo MKUFUNZI

Tarehe 23/11/2021

MAJIRIWA (FUNDI)

Saini: ..........................................

Jina: ELIUDI JOHN MLENZA

Cheo: FUNDI

Tarehe: 23/11/2021

SHAHIDI WA MAJIRIWA (FUNDI)

Saini: ..........................................

Jina: JACOB ANDREW HUNGELA

Cheo: FUNDI

Tarehe: 23-11-2021.

| | | |
|---|---|---|
| | Usukaji wa mifumo ya tehama awamu ya kwanza - Conduit na Box | 800,000.00 |
| | Usukaji wa mifumo ya tehama awamu ya pili (2nd fix)-fittings | 1,200,000.00 |
| | **Jumla ndogo Tehama** | **2,000,000.00** |
| | | |
| J. | **Mifumo ya maji safi na taka (Water Supply and Sewage system)** | |
| | Ufungaji bomba awamu ya kwanza (Kuchimbia bomba) | 500,000.00 |
| | Ufungaji bomba awamu ya pili (2nd fix) -fittings | 700,000.00 |
| | Uchimbaji wa mashimo ya maji taka (Septic na Soak pit) | 1,800,000.00 |
| | Ujenzi wa mashimo ya maji taka na chemba zake ikiwa ni pamoja nakufanyia finishings | 2,000,000.00 |
| | **Jumla ndogo Mifumo ya maji safi na maji Taka** | **5,000,000.00** |
| | | **SUMMARY** |
| A | Gharama za Msingi (Substructure) | 12,800,000.00 |
| B | Gharama za Kunyanyua Jengo(Superstructure) | 15,800,000.00 |
| C | Gharama za Kuezeka | 2,100,000.00 |
| D | Gharama za Kufutisha Milango | 800,000.00 |
| E | Gharama za Kufutisha Madirisha | 1,000,000.00 |
| F | Gharama za Umaliziaji (Finishing) | 9,950,000.00 |
| G | Gharama za Rangi na Mapambo | 4,150,000.00 |
| H | Gharama za Umeme | 1,500,000.00 |
| I | Gharama za Mifumo ya Tehama | 2,000,000.00 |
| J. | Gharama za Mifumo ya Maji Safi na Maji Taka | 5,000,000.00 |
| **JUMLA KUU YA GHARAMA ZA KAZI ZA UJENZI** | | **55,100,000.00** |